

Sala ya Asubuhi ya kila siku

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · January 17, 2016

Sala za Katoliki: Sala Muhimu Kwa Mkristu Mkatoliki · #sala · #Sala za Ibada · #Sala za Kushukuru · #Sala za Maombi

Ee Baba yetu Mungu mkuu, umenilinda usiku huu. Nakushukuru kwa moyo, ee Baba, Mwana na Roho. Nilinde tena siku hii, niache dhambi nikutii. Naomba sana Baba wee, baraka yako nipokee. Bikira safi, Ee Maria nisipotee nisimamie. Mlinzi mkuu malaika wee kwa Mungu wetu niombe, nitake nitende mema tu na mwisho nije kwako juu. Amina. NIA NJEMA.

Kumueshimu Mungu wangu, namtolea roho yangu. Nifanye kazi nipumzike, amri zake tu nishike. Wazo, neno, tendo lote namtolea Mungu pote Roho, Mwili chote changu. Pendo na uzima wangu. Mungu wangu nitampenda wala dhambi sitatenda. Jina lako nasifia, utakalo hutimia kwa utii navumili. Teso na matata pia, nipe Bwana neema zako, niongeze sifa yako. Amina. SALA YA MATOLEO.

Ee Yesu kwa mikono ya Bikira Maria, na kwa maungano na sadaka yako kuu. Ninakutolea sala, matendo, masumbuko na furaha zangu zote za leo. Ee Yesu ufalme wako utufikie. Amina. BABA YETU.

Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe. Ufalme wako ufike. Utakalo lifanyike duniani kama mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kila siku. Utusamehe makosa yetu, kama tunavyo wasamehe na sisi waliyo tukosea. Usitutie katika kishawishi, lakini utuopoe maovuni. Amina. SALAMU MARIA.

Salamu Maria, umejaa neema Bwana yu nawe, umebarikiwa kuliko wanawake wote, na Yesu mzao wa tumbo lako amebarikiwa. Maria mtakatifu Mama wa Mungu, utuombe sisi wakosefu sasa na saa ya kufa kwetu. Amina. KANUNI YA IMANI.

Nasadiki kwa Mungu, Baba Mwenyezi, muumba mbingu na dunia. Na kwa Yesu Kristu Mwanaye wa pekee, Bwana wetu aliyetungwa kwa Roho Mtakatifu, akazaliwa na Bikira Maria, akateswa kwa mamlaka ya ponsyo Pilato, akasulibiwa, akafa, akazikwa, akashukia kuzimu siku ya tatu akafufuka katika wafu, akapaa mbinguni amekaa kuume kwa Mungu Baba Mwenyezi, toka huko atakuja kuwahukumu wazima na wafu. Nasadiki kwa Roho Mtakatifu, kanisa takatifu katoliki ushirika wa Watakatifu, maondoleo ya dhambi, ufufuko wa miili na uzima wa milele. Amina. AMRI ZA MUNGU.

1. Ndimi Bwana Mungu wako, usiabudu miungu wengine. 2. Usilitaje bure jina la Mungu wako. 3. Shika kitakatifu siku ya Mungu. 4. Waheshimu Baba na Mama upate miaka mingi na heri duniani. 5. Usiue. 6. Usizini. 7. Usiibe. 8. Usiseme uwongo. 9. Usitamani mwanamke asiye mke wako. 10. Usitamani mali ya mtu mwingine. AMRI ZA KANISA.

1. Hudhuria misa takatifu domonica na sikukuu zilizo amuliwa. 2. Funga siku ya jumatano ya majivu, usile nyama siku ya Ijumaa kuuu. 3. Ungama dhambi zako walau mara moja kwa mwaka. 4. Pokea Ekarist takatifu hasa wakati wa Pasaka. 5. Saidia kanisa katoliki kwa zaka. 6. Shika sheria katoliki za ndoa. SALA YA IMANI.

Mungu wangu, nasadiki maneno yote linayo sadiki na kufundisha kanisa katoliki la Roma kwani ndiwe uliye fumbuliwa hayo, wala hudanganyiki na wala hudanganyi. Amina. SALA YA MATUMAINI.

Mungu wangu,natumaini kwako nitapewa kwa njia ya Yesu Kristu,neema zako duniani na utukufu mbinguni.Kwani ndiwe uliyeagana hayo nasi nawe mwamini.Amina. SALA YA MAPENDO.

Mungu wangu,nakupenda zaidi ya chochote, kwani ndiwe mwema ndiwe mwenye kupendeza. Nampenda na jirani yangu kama nafisi yangu kwa ajiri yako.Amina. SALA YA KUTUBU.

Mungu wangu,nimetubu sana dhambi zangu kwani ndiwe mwema,ndiwe mwenye kupendeza wachukizwa na dhambi. Basi sitaki kukosa tena nitafanya kitubio,naomba neema yako nipate kurudi.Amina. SALA KWA MALAIKA MLINZI.

Malaika mlinzi wangu,unilinde katika hatari zote za Roho na za Mwili.Amina. MALAIKA WA BWANA.

K.Malaika wa Bwana alimpasha habari Maria. W.Naye akapata mimba kwa Roho mtakatifu.

K.Ndimi mtumishi wa Bwana. W.Nitendewe ulivyo nena.

K. Neno la Mungu akatwaa Mwili. W. Akakaa kwetu.

K. Utuombee Mzazi Mtakatifu wa Mungu. W. Tujaliwe ahadi za Kristu.

Tuombe.

Tunakuomba Ee Bwana utie neema yako mioyoni mwetu ili sisi tuliyojuwa kwa maelezo ya malaika kwamba, Kristu mwanao amejifanya mtu kwa mateso na msalaba wake. Tufikishwe kwenye utukufu wa ufufuko. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristu Bwana wetu.Amina. ATUKUZWE BABA.

Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu,kama mwanzo na sasa na siku zote na milele.Amina.

K. Moyo Mtakatifu wa Yesu W.Utuhurumie.

K. Moyo safi wa Bikira Maria. W. Utuombee.

K. Mtakatifu Yosefu. W. Utuombee.

K. Watakatifu somo wa majina yetu. W. Mtuombee.

K.Watakatifu wote wa Mungu. W.Mtuombee.